


TANGAZO

Mfuko wa Udhamini wa Kumbukumbu ya Mwalimu Julius Nyerere unaosimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania unatangaza nafasi za udhamini (Scholarships) wa masomo ya elimu ya juu kwa mwaka 2021/2022.

Ufadhili huu, unalenga kuongeza hamasa na ufaulu kwa wanafunzi wa kike hapa nchini katika **masomo ya Hisabati na Sayansi.** Unajumuisha gharama zote za ada, pesa za kujikimu (malazi na chakula), mafunzo ya vitendo na vifaa vya kujifunzia ikiwemo kompyuta mpakato (Laptop). Utatolewa kwa wanafunzi **kumi (10)** raia wa Tanzania wenye ufaulu wa kiwango cha juu waliosajiliwa katika vyuo vikuu vinavyotambulika nchini.

Kwa **Shahada ya Kwanza,** ufadhili utatolewa kwa wanafunzi waliohitimu kidato cha sita mwaka 2021 na wenye ufaulu wa daraja la kwanza miongoni mwa wanafunzi kumi bora kitaifa, katika makundi yafuatayo:

a) Wanafunzi wa **kike tu**, waliochaguliwa kuendelea na masomo ya elimu ya juu ya **Shahada ya Kwanza** katika fani ya **Hisabati au Sayansi**.

b) Wanafunzi wa **kike na kiume,** waliochaguliwa kuendelea na masomo ya elimu ya juu ya **Shahada ya Kwanza** katika fani ya **Hisabati, Sayansi**, **Uchumi, TEHAMA, Uhasibu au Fedha.**

Orodha ya wanafunzi kumi bora itapatikana toka Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA).

Kwa **Shahada ya Uzamili,** ufadhili utatolewa kwa wanafunzi wa **kike na kiume**, wenye ufaulu wa juu katika shahada ya kwanza kujiendeleza katika fani ya **Hisabati, Sayansi, Uchumi, TEHAMA, Uhasibu au Fedha** Maombi yanakaribishwa.

Kwa maelezo zaidi kuhusu udhamini huo na fomu za maombi tembelea tovuti ya Benki Kuu ya Tanzania: **www.bot.go.tz**.

Fomu pia zinapatikana Benki Kuu katika ofisi za Makao Makuu Dodoma, Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Zanzibar, Mbeya, na Mtwara.

Limetolewa na:
Mwenyekiti,
Kamati ya Mfuko wa Udhamini wa
Kumbukumbu ya Mwalimu Julius Nyerere,
Benki Kuu ya Tanzania,
2 Mtaa wa Mirambo,
11884, **DAR ES SALAAM.**